# Maana katika Majina ya Wabena nchini Tanzania

Mnata Resani

**Ikisiri**

Jina, kulingana na Plato, ni aina ya maneno na ni njia pekee ya kurejelea dhana au kitu. Maana ilihusishwa na jina na ujinaishaji (Resani, 2015). Kutokana na umuhimu wa jina, binadamu wamepewa na kupeana majina kama kitambulisho cha kuwatambulisha miongoni mwa jamii husika. Kila jamiilugha ina majina ambayo huitambulisha zaidi, lakini ukweli unabaki kuwa kila jina apewalo mtu lina maana na athari kwa mhusika. Katika makala hii tumejadili maana ya majina wapewayo watu wa jamii ya Wabena. Kabla ya ufafanuzi wa majina hayo imeelezwa historia ya Wabena ikionyesha shughuli zao za kiuchumi, eneo lao la kijiografia wanalopatikana na majirani wanaowazunguka. Makala kwa undani inaeleza chanzo cha majina, maana na athari ya majina kwa mwenye jina katika jamii ya Wabena mkoani Njombe nchini Tanzania.

## 1.0 Utangulizi

Jina ni kipengele muhimu cha maisha, utambulisho na utamaduni wa binadamu katika jamii mbalimbali. Jina ni neno linalotaja kitu (mfano kiti, meza, na chungu), kiumbe (mfano mtu, ndege, mnyama au mtu), sehemu (mfano Tanzania, Kinondoni na Tabora), tendo (mfano kusukuma na uainishaji) na hali (mfano majonzi na furaha) (Massamba, 2004). Majina yamegawanyika katika makundi kama vile majina jumuishi (majina ya kawaida), majina mahususi (majina ya pekee) na majina ya makundi (majina ya jamii) (Kihore na wenzake, 2009; Buberwa, 2010). Kulingana na mgawanyo huu wa majina, Resani (2012) akielezea majina ya pekee kutoka katika jamii ya Wakurya, anasema kuwa jina ni neno ambalo huwa linabeba elementi mbalimbali katika jamii. Aidha, jina huwa na nguvu na athari kwa mwenye nalo na mengi ya majina maana yake huwa na kitu au dhana ambayo hukumbusha jamii matukio mbalimbali ya kijamii. Jina huwa na chanzo chake katika jamii na kupitia jina unaweza kujua jinsi ya mtu/mwenye jina. Makala hii inachunguza majina ya Wabena pamoja na maana zake katika jamii husika. Katika utangulizi wa makala hii tumeeleza historia na asili ya Wabena huku ikionyesha shughuli zao za kiuchumi, eneo lao la kijiografia, lugha na lahaja zake. Sehemu ya pili ndiyo kiini cha makala yetu ambapo utaratibu wa kupeana majina katika jamii husika ikiwemo muktadha ulioibua majina hayo na maana ya majina hayo katika jamii hiyo unatolewa. Mwisho kabisa ni hitimisho.

## 1.1 Historia ya Lugha ya Kibena

Kibena ni lugha ya Kibantu nchini Tanzania inayozungumzwa na Wabena wanaopatikana katika Mkoa wa Njombe. Katika sensa iliyofanyika mwaka 2012 idadi ya wasemaji wa Kibena ilikadiriwa kuwa na watu takribani 702,097 ambapo wanaume ni 329,359 na wanawake ni 372,738. Mkoa wa Njombe una wilaya za Ludewa,

Wanging'ombe, Makete na Njombe. Wabena ni jamii ya watu wanaoishi hasa katika kata za Lyamkena, Mjimwema, Igima, Imalinyi, Mdandu na Kidugala (Kibiki, 2013). Asili ya neno "bena" ni kuvuna au kuchuma mali au kitu cha thamani. Baadhi ya watu hudai kuwa neno hili linatokana na kitendo cha kuvuna ulezi (*hubena wuledzi*). Neno hili liliibuka kutokana na shughuli kuu ya Wabena ya kuvuna ulezi inayofanywa na wenyeji wa mkoa huo. Mathalani, Nyagava (1988) anasisitiza kuwa katika jamii na utamaduni wa Kibena istilahi "Bena" inatokana na shughuli za kuvuna ambapo neno *hubena* humaanisha kuvuna kwa kutumia mikono; kwa mfano kuvuna mahindi. Hivyo, watu wanaofanya shughuli hii ya kuvuna huitwa *avabena*. Kwa upande mwingine, Mbogela (2011:38) anatanabahisha kuwa kuna watu wengine hudai neno "bena" limetokana na shughuli ya kuchimba chumvi, yaani kuchuja na kuitenganisha na makapi ijulikanayo kama '*hubena umunyo*', dhana ambayo hutumika hadi sasa. Kwa ujumla, neno "Bena" limetokana na shughuli za uzalishaji mali katika jamii hiyo.

Lugha nyingine zilizo karibu na Kibena ni Kihehe na Kisangu, ambazo zipo upande wa Kaskazini mwa eneo la Wabena (wilaya ya Njombe), Kikinga na Kiwanji zipo upande wa Magharibi mwa eneo la Wabena, Kipangwa na Kingoni zipo upande wa Kusini, na upande wa Mashariki mwa eneo la Wabena kuna Kipogolo.

## 1.2 Asili ya Wabena na Shughuli zao za Kiuchumi

Ubena ni eneo lote linalokaliwa na watu waishio katika wilaya ya Njombe na maeneo yanayozunguka wilaya hiyo. Ubena inajumuisha eneo la Magharibi mwa Bonde la mto Mpangali (Usangu), milima ya Livingstone kuelekea kusini hadi bonde la Luhudhzi, yaani Usangu Mashariki. Eneo hili linapatikana mistari ya latitudo 7.5 na 9.8 kusini na mistari ya longitudo 34.4 na 36 Mashariki (Nyagava, 1988:47). Eneo kubwa la Ubena liko nyanda za juu Kusini, kiasi cha mita 1500-2600 juu ya usawa wa bahari. Eneo hili chanzo chake huanzia Mto Ruaha mkuu na Kilombero, yote ikianzia Milima ya Livingstone. Mito midogo inayotiririsha maji yake katika mito hiyo mikubwa ni pamoja na Mpangali, Balali, Ruaha mdogo, Kihanzi, Manyara na Luhudhzi. Hali ya hewa ya Ubena ni ya Kitropiki iliyoathiriwa na mwinuko mkubwa kutoka usawa wa bahari. Kwa hiyo, kuna baridi kali sana hasa miezi ya Juni hadi Agosti na mvua hunyesha wakati wa masika hasa miezi ya Desemba mpaka Aprili (Nyagava, 1994).

Enhret (1958) akinukuliwa na Nyagava (1988) anaeleza kuwa Wabena walitoka pwani ya Afrika Mashariki wakielekea uwanda wa juu wakati wakitafuta chanzo cha Mto Rufiji kupitia Ulanga na Kilombero. Hatimaye wakafika na kukaa eneo linaloitwa *Nyumbanitu* "Nyumba nyeusi". Kwa mujibu wa utafiti wetu wa uwandani, historia inaeleza kuwa:

> Wabena wa awali walipanga mahali palipoitwa *Nyumbanitu*, Kaskazini mwa chanzo cha Ruhuye (Ruhuji) si mbali na Ndandu (mdandu), mji uliokuwa makazi ya viongozi wakuu wa Wabena. Wengine walikwenda kukaa katika sehemu za milimani kaskazini mwa ziwa Malawi, wakawa Wasafwa, wengine hasa kutoka Ukinga, walienea Kusini wakawa Wapangwa na walioenea


> katika uwanda wa juu ng'ambo ya mto Ruhuye (Ruhuji) waliendelea kuitwa Wabena na eneo likaitwa Ubena. *Nyumbanitu* ni pango lililoko katika msitu mkubwa ambalo linatumika kwa matambiko ya Wabena hadi leo na limekuwa kivutio kikubwa sana katika utamaduni wa Wabena. Eneo hilo lina msitu mkubwa wenye wanyama wa kila aina na mtu hupaswi kuingia katika pango hilo bila kuruhusiwa na ukifanya hivyo unaweza kupotelea huko huko ndani ya pango (Nuso na Mgaya, 2015, Masimulizi ya mdomo).

Kibiki (2013) anaeleza kuwa jamii ya Wabena ilianza kuimarika baada ya kila ukoo kujishughulisha na kilimo ambacho kiliifanya jamii hiyo iweze kutulia mahali pamoja na kuanza kuwa na uongozi wa kisiasa hata kabla ya kipindi cha biashara ya masafa marefu. Viongozi waliitwa watwa na walitawala koo mbalimbali za Kibena. Mathalani, *Mbeyela* alitawala Ikilavungi, *Nyanguvila* alitawala Mfikika (Lupembe), *Mlelwa* alitawala Nyikolowe na *Mligo* alitawala Usovi. Viongozi hawa walitawala kati ya miaka ya 1850 katika mkoa wa Njombe ya leo.

Makabila makubwa ya wenyeji mkoani Njombe ni Wabena, Wakinga na Wapangwa. Kabila la Wabena liko wilaya ya Njombe eneo la Malangali likiwa linapakana na wilaya ya Ulanga na wilaya ya Kilombero (Mkoa wa Morogoro). Wakinga wako wilaya ya Makete na Wapangwa wako eneo la Malangali. Kuna makabila madogo kama vile Wakisi na Wamanda ambao kwa ujumla wao wanachukua asilimia 6 iliyosalia ya watu wa mkoa wa Njombe (Nyagava, 1994). Kufuatana na uainishaji wa lugha za Kibantu wa Malcom Guthrie (1948), lugha ya Kibena iko katika kundi la G 60.

Hapo mwanzoni, Wabena walijishughulisha na ufugaji wa ng'ombe, biashara ya pembe za ndovu na watumwa wakati wa biashara ya watumwa. Kwa sasa, shughuli muhimu za kiuchumi zinazofanywa na Wabena wa mkoa wa Njombe ni kama kilimo cha mahindi, ngano, viazi mviringo na wengi hutegemea mavuno ya mbao kutokana na miti ya mipeinesi (miti ya mbao). Kilimo cha miti ya mbao kimechangia sana katika uchumi wa Wabena wengi wanaoishi katika mkoa wa Njombe na wilaya zake zote. Kwa sasa watu wengi wanajishughulisha zaidi na kilimo cha umwagiliaji wa viazi, ambapo awali viazi kilikuwa kilimo cha msimu wakitegemea mvua jambo linalorudisha nyuma maendeleo kwa wakulima wa Njombe.

**Ramani ya Mkoa wa Njombe Kuonyesha Eneo la Wabena na Majirani Zao (Nyagava, 1988)**




**1.3 Hadhi ya Lugha ya Kibena Sasa**

Hadhi ya lugha ya Kibena katika mkoa wa Njombe ni kubwa kwa sababu inatumiwa na wazungumzaji katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi ambazo jamii hufanya kila siku. Kwa mfano, lugha ya Kibena inatumika sana katika vikao vya ukoo, familia na katika mikutano ya vijiji. Lugha ya Kibena inatumika katika shughuli za kiuchumi kama kilimo ambapo wakulima hutumia nyimbo za kikabila ili kuleta hamasa katika kazi mfano, kuna nyimbo kama vile "*iligimilo ni nyengo ye babuo nu nyoho ukangalage*

*ulimage ulaliya humwaha*" wakiwa na maana kuwa wakati wa kilimo shika jembe na fyeko ukalime utakula mwakani.

Hivyo, lugha ya Kibena hadhi yake ni kubwa sana katika matumizi ya shughuli za jamii ya Wabena wanaoishi mkoa wa Njombe na maeneo mengine ambako Wabena wanapatikana. Kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya vijijini Kibena hutumika kama lugha mama majumbani katika mawasiliano ya kawaida hususani na wazee wa makamo pamoja na watoto walio chini ya miaka 10. Makundi ya vijana na watu wa umri wa kati, hususani walioenda shule (wasomi), wamechangamana sana na lugha zingine kama Kiswahili na Kiingereza. Hivyo hii ni dalili njema kwa Kibena kuwa kitaendelea kwa muda mrefu kuzungumzwa.

Lugha ya Kibena ni pana na ina lahaja mbalimbali ambazo zimepata kuainishwa na wataalamu wengine. Kilimile (2009) anasema lugha ya Kibena ni tajiri sana kwa maneno na ni pana sana ikiwa na lahaja kuu tano ambazo ni: Kikilavwungi inapatikana maeneo ya Ilembula, Kisovi inapatikana katika maeneo kuanzia Lusisi hadi Makambako, Kimaswamu kinazungumzwa Imalinyi, Njombe mjini na sehemu ya kata ya Mdandu, Kilupembe kinazungumzwa Lupembe na lahaja ya Kimavemba inayozungumzwa Uwemba na sehemu ya tarafa ya Igominyi ambayo si ya Maswamu. Makala hii inatumia lahaja ya Kimavemba ambayo haijaandikwa na watafiti wengi katika lugha ya Kibena.

Lugha ya Kibena ni moja lakini tofauti ni ndogondogo ambazo zipo katika matamshi, kwa mfano lahaja zote zinakaza "dz" isipokuwa Kikilavwugi ambapo "dzi" inatamkwa kama "dji" (tazama maneno kama *umuhudji* (mchuzi), na katika Kilupembe inatamkwa kama "chi" (tazama maneno *umuhuchi* (mchuzi), na *achile* (amekuja). Aidha, neno kama "adjile' wengine hulitamka kama adzile (amekuja). Tofauti nyingine ni ya kutumia mofu [k] na [h] kwa mfano katika maneno *kamwene/hamwene* (salamu mnayopeana na mtu unapokutana naye kama mlikuwa hamjaonana katika siku) na *kukalangidza/hukalangidza* (kukaangiza). Hivyo, /k/ na /h/ ni alomofu za mofimu moja yaani sauti ambazo hazibadili maana katika maneno mawili yenye maana moja zinamotumika.

## 2.0 Majina ya Watu katika Jamii ya Wabena

Katika kabila la Wabena majina ya ukoo yaliyo mengi yanaanza na mofu [m]; kwa mfano katika koo zifuatazo: *Mgaya*, *Msemwa*, *Mligo*, *Mnenuka*, *Msigwa*, *Mswata*, *Mlowe*, *Mgeni*, *Mbilinyi*, *Mgina* na mengine jamii ya hayo (Nyagava, (1988). Hata hivyo, hali kama hii haipo tu kwa lugha ya Kibena bali katika baadhi ya makabila kwa mfano katika lugha ya Kipare koo nyingi zinaanzia na mofu [m] mfano katika koo kama vile: *Msuya*, *Mshana*, *Mmbaga*, *Mzirayi*, *Mfinanga*, *Mchomvu*, *Msangi* na mengine jamii ya hayo.

Baadhi ya majina katika jamii lugha ya Wabena yana asili ya lakabu, yanatokana na matukio na mengine ni ya kurithi. Kwa mujibu wa Wamitila (2010:173-174) lakabu ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya wanajamii hupewa au hujipa wenyewe ukubwani. Majina haya hutokana na sifa au wasifu wao wa kimwili, kiukoo, kijadi, kitabia au kimatendo. Aghalabu, majina haya hutumia tamathali kama sitiari kusifu mtu au hata kumkejeli. Mulokozi (1996:42) akifafanua maana ya lakabu anasema kuwa lakabu ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipatia kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba au kimatendo. Majina haya huwa ni neno au mafungu ya maneno yenye maana iliyofumbwa. Mara nyingi humsifia mhusika, lakini mengine humkosoa au hata kumdhalilisha mtu. Hivyo, tunaweza kusema kuwa lakabu ni majina ambayo hutolewa kulingana na hali halisi ya mtu, yaani tabia yake, maumbile yake na hata ukoo wake alikotokea. Aidha, lakabu ni kipera cha fasihi simulizi kinachopatikana katika utanzu wa semi. Ni fumbo jina analotumia mtu, mwandishi au msanii ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Hivyo, majina yenye asili ya lakabu ni muhimu sana katika jamii na ni sehemu ya utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika pamoja na Ubena kwa ujumla.

Katika jamii ya Wabena kuna changamoto mbalimbali kuhusiana na utamaduni. Mathalani, historia ya jamii hiyo, uchumi wa jamii, lugha na dhima ya lakabu katika kupeana majina ya asili. Inasemekana kwamba hakuna kumbukumbu zinazohusu majina ya asili, hii ni kwa sababu ya mwingiliano wa jamii mbalimbali hasa wageni kutoka nje, ambapo wanajamii hupenda kuiga majina bila kujua maana na asili ya majina hayo. Hata hivyo, kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika za kupeana majina ya kurithi kutoka kwa wazee, Wabena wana utamaduni wa kurithishana majina. Jina moja huweza kutolewa kwa wanajamii kutoka kizazi kimoja na kingine, na hii hushabihiana kabisa na falsafa ya uviringo ya Waafrika. Jina huweza kuzunguka katika familia, kwa kufanya hivyo wanajamii huamini kuwa mtoto akirithishwa jina la babu/bibi katika ukoo kunamfanya aendelee kuishi hata kama babu/bibi au ndugu huyo alishakufa. Wabena pia huamini kuwa kurithishana majina ni njia pekee ya kumuenzi ndugu aliyekufa hivyo majina hayo hubakia kama kumbukumbu ya ndugu aliyekufa na ni sehemu ya kutunza matukio yaliyotokea wakati huo (Hountondji, 1977).

### 2.1 Majina katika Jamii ya Wabena: Taratibu, Muktadha na Maana zake

Uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi wazazi walipenda sana kuwapa watoto majina ya watu waliokuwa na wasifu mzuri na ambao ni hodari. Mathalani wakulima hodari, wawindaji hodari, wahunzi wazuri, matajiri wakubwa na watawala wa jadi (machifu). Kwa upande mwingine jamii ya Wabena waliepuka sana kutoa majina ya watu walioonekana wana tabia mbaya katika jamii zao kama vile wizi, utundu, ubakaji na uzembe wa kazi. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa ni kuondokana na urithi mbaya. Vilevile, wengine huweza kurithi majina ya ndugu zao walio hai au waliofariki; lengo ni kutunza kumbukumbu za ndugu hao. Pia, wazazi walizingatia kuwa majina wanayowapatia watoto wao yanasadifu tabia zao, kwa kufanya hivyo waliamini kuwa jina analopewa mtoto ni la kumsifia, kumkosoa, kumliwaza na pengine kumtia hamasa

ya kufanya mambo fulani makubwa katika jamii. Katika jamii ya Wabena utoaji wa majina umetawaliwa na miktadha kadhaa na utamaduni wa jamii husika. Ufafanuzi wa baadhi ya miktadha au asili ya majina hayo ni kama ifuatavyo:

**a) Majina Yanayotokana na Shughuli za Kiuchumi**

Shughuli za kiuchumi katika jamii ni sababu mojawapo ya kupeana majina. Kwa mfano, jina *Twihuvila* maana yake ni tunamtegemea. Mwenye jina hili huwa ni mtu ambaye ni tegemeo katika familia kutokana na uchapakazi wake. Pia, jina *Mutataluvanja* humaanisha kuwa ni mtu ambaye anamiliki sehemu kubwa ya ardhi kwa shughuli za kilimo. Mwenye jina hili mara nyingi huwa ni hodari na mwenye kujishughulisha na kilimo, hivyo jina husadifu sifa au tabia ya mtu huyo. Jina hili ni la kiume hivyo hupewa wanaume tu. Hii huonyesha pia kuwa ardhi ni kitu muhimu sana kwa jamii maana wanaume ndio hurithi ardhi lakini sio kwa wanawake.

Jina jingine ni *Khimetelo*, maana yake ni kifaa kinachotumika wakati wa mavuno (humeta), kwa mfano, kikapu, mundu au kisu. *Humeta* humaanisha kushindilia kwa wingi katika kifaa fulani, yaani kujaza sana. Jamii ya Wabena huweza kumpa mtoto jina hili kwa lengo la kuitambulisha jamii kuwa mtoto alizaliwa kipindi cha mavuno mengi ukilinganisha na miaka kadhaa iliyopita. Jina hili huweza kumfanya mtu anayepewa kuwa na shauku na juhudi katika uzalishaji mali.

Kwa kuwa shughuli za kilimo ni uti wa mgongo katika jamii ya Wabena hivyo watu wenye tabia zenye kurudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi huakisiwa katika majina haya. Mathalani, tabia ya uvivu miongoni mwa wanajamii hufanya kupewa majina kama vile *Mukhemedzi*, *Sangamela*, *Lufuna* na *Mulimilavangi*. *Muhemedzi* ni jina lenye maana ya mtu mwenye tabia ya kuombaomba kwa ndugu, jamaa na kwa majirani kama vile chakula wakati ana nguvu za kufanya kazi na kuweza kujipatia kipato. Hivyo, mtu au mtoto mwenye tabia hizo hupewa jina hili ili kutambulishwa katika jamii kuwa ni mvivu. Jamii pia hufanya hivyo ili kuondoa tabia ya uvivu kwa familia inayofuata. *Sangamela* pia ni jina lenye maana ya kusubiri kupewa bila ya mtu kujishughulisha katika kufanya kazi za uzalishaji. Pia, *Mulimilavangi* ni jina analopewa mtoto aliyezaliwa na wazazi wenye tabia au hali ya kupenda kulima kidogo tu katika mashamba yao na muda mwingi hutumia kulima vibarua kwa watu wengine kwa lengo la kupata mlo wa wakati huo. Kwa Kibena *mlimila* maana yake ni ‘mkulima’ na *vangi* maana yake ni ‘wengine’ au ‘anayelimia watu wengine’ (kibarua). Jina hili hutolewa ukubwani mtu anapokuwa na umri kuanzia miaka kumi na mitano, huwa ni la kukejeli watu wenye tabia ya uvivu na kwamba wanajamii hutoa majina haya ili kubadili tabia zao. Katika jamii ya Wabena anayepewa jina hili huwa ameonekana kuwa ni mvivu, hivyo jina hili linampa hamasa ya kufanya kazi kwa bidii na kuondokana na uvivu. Pia, jina hili hubaki kumbukumbu ya tabia ya mtoto kwa wazazi wake na watoto atakaowazaa ili kutoa fundisho kwa watoto na watu wengine kuepukana na tabia za uvivu, uzembe na kutojithamini.

**b) Majina Yanayotokana na Kuzaliwa Nje ya Ndoa**

Wapo watoto ambao mama zao hawakupata kuolewa au kabla ya kuolewa walipata kuwa na watoto. Mathalani, jina *Tumwanukye* maana yake ni tumempokea. Jina hili hupewa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa, yaani bila kufuata taratibu za kuoana ambazo zinakubalika katika jamii. Majina haya ni machache kulinganisha na majina mengine hii ni kutokana na umuhimu wa kuwa na ndoa katika jamii husika. Kwa kawaida ni jina ambalo humfedhehesha mwanamke kama onyo kwa wanawake kuacha mapenzi kabla ya ndoa. Hivyo ikithibitishwa kuwa mtoto huyo aliyezaliwa ni kweli kuwa si mtoto wa mume aliyemuoa mwanamke (mama wa mtoto), basi anaweza kupokelewa katika familia na kupewa jina *Tumwanukye* yaani tumempokea.

**c) Majina ya Watoto Wanaozaliwa baada ya Majonzi katika Familia**

Wapo watoto waliozaliwa wakati wa msiba unaohusu familia ya mtoto aliyezaliwa. Watoto wa kike waliozaliwa katika kipindi hiki huweza kuitwa *Lunyodzi*, *Lunyamadzo*, *Dzivembela* na wa kiume huitwa *Lugelekha* au *Mombwi*. Hivyo dhima ya kuwapa majina hayo ni kuweka kumbukumbu ya ndugu zao waliofariki na wakati mwingine huamini kuwa ni tahadhari kwa miungu ili mtoto aliyezaliwa asije akafa kama walivyofariki ndugu zake waliotangulia. *Lunyodzi* humaanisha machozi yanayotokana na kulia wakati wa msiba na mara nyingi wanawake ndio hulia na kutoa machozi wakati wa msiba. *Lunyamadzo* humaanisha kunyamazisha, kuliwaza na kufariji mtu mwenye majonzi. Hivyo, *Lunyamadzo* ni kitendo cha kumliwaza na kumnyamazisha mtu aliyepatwa na tatizo fulani ili aache kulia au kusononeka moyoni. Katika jamii ya Wabena mtoto hupewa jina hilo wakiamini kuwa mtoto aliyezaliwa atakuwa tulizo kwa mama ambaye mara nyingi hujifungua watoto na wanafariki. *Dzivembela* ni jina lingine lenye maana usilie tena, yaani kwamba mtoto huyu ni tulizo na mama yake aache kulia na kuhuzunika. Majina haya hupewa mtu wa jinsi ya kike au ya kiume.

Kwa upande wa majina ya watoto wa kiume nayo hubeba maana fulani kwa watoto wanaopewa majina hayo. Kwa mfano, *Mombwi* ni shimo refu ambalo huchimbwa kwa lengo la kuzikia watu waliokufa. Kwa kawaida mtoto wa kiume hupewa jina hili kwa kuwa katika jamii za Wabena wanaume ndio huhusika katika kuchimba kaburi pindi mtu anapokufa. Hivyo jina hili akipewa mtoto katika mazingira hayo huwa ni tahadhari kwa mizimu (wafu au wahenga) ili kuepusha kifo kwa mtoto mwenye jina husika. *Lugelekha* ni udongo uliokusanywa na kufanya tuta ambalo hutumika kupanda kama vile mihogo, mahindi, viazi na mengine kama hayo. Vilevile *Lugelekha* katika jamii ya Wabena ni ule udongo ambao hukusanywa juu ya shimo alilozikwa mtu aliyekufa ambapo tuta hilo ndilo huitwa kaburi. Hivyo jina hili hupewa mtoto ili kuweka tahadhari kwa mizimu kuwa hatuogopi kifo lakini mtoto aliyezaliwa aendelee kuwa hai.

Si hivyo tu, bali kuna majina mengine kama vile *Godzihove* na *Matakgilo*. *Godzi* humaanisha tengenezwa, weka vizuri au hudumia na *Hove* ni ndege arukaye mwenye

rangi nyeusi na nyeupe aitwaye Kunguru. Ndege huyo hupenda kula mizoga ya wanyama wengine. Hivyo jina *Godzihove* lina maana ya kuhudumiwa na kunguru. Jina hili hupewa mtoto aliyezaliwa na mama au wazazi ambao watoto wao wengine wa kwanza walishafariki hivyo huwa na hofu kuwa pengine hata huyo aliyezaliwa atakufa na wakati wa uzee wasiwe na mtu wa kuwasaidia. Vilevile huamini kuwa wasipokuwa na watoto wa kuwahudumia watakapokuja kufariki wataliwa na kunguru. Lengo la kumpa jina hili mtoto ni kuomba dua kwa mizimu ili mtoto aliyezaliwa asife. *Matakgilo* ni jina analopewa mtoto aliyezaliwa katika jamii ya Wabena likiwa na maana ya eneo lililotengwa au linalotumika kuzika watu tu. Jina hili hupewa mtoto ambaye amezaliwa katika familia ambayo imekuwa na tatizo la kufiwa kila mara hivyo mtoto huyo hupewa jina hilo kwa lengo la kutunza kumbukumbu ya matukio ya misiba iliyoikumba familia husika. Athari ya jina hili katika jamii ya Wabena ni kwamba mtoto anayepewa jina hili hurithi matatizo aliyokuwa nayo bibi au babu wa mtoto huyo hata kama aliowarithi wapo au walishafariki. Hii ni kuonyesha kuwa, falsafa ya Kiafrika huamini katika nguvu zilizomo ndani ya jina na kwamba majina humfanya mtu akaonekana au kuishi kulingana na jina lake lilivyo (Resani, 2012).

**d) Majina Yanayotokana na Nafasi/Upekee wa Mtoto katika Familia**

Pia, kuna majina kama vile *Atulongolye* na *Lutengamaso* ambayo hutolewa kutokana na nafasi na upekee wa mtoto katika familia husika. Kwa mfano, *Atulongolye* humaanisha kuwa ametutangulia jina hili hupewa mtoto wa kike ambaye ni wa kwanza kuzaliwa. Katika jamii ya Wabena humpatia mtoto wa kike jina hili kwa lengo la kumtambulisha mtoto husika kuwa ni wa kwanza katika uzao wa familia. *Lutengamaso* maana yake ni amani, suluhu, sawazisha au furaha. Jina hili hupewa mtoto wa kiume ikiwa waliomtangulia kuzaliwa ni watoto wa kike. Katika jamii ya Wabena wanathamini sana mtoto wa kiume wakiamini kuwa ndiye kiongozi katika ukoo wao. Endapo ikatokea katika familia fulani mama amefululiza kuzaa watoto wa kike tu basi wazee na wanaukoo huwa na hofu. Familia ikipata mtoto wa kiume basi ndiyo hupewa jina tajwa na lengo ni kuweka kumbukumbu endapo ukoo haukuwa na amani basi wanaamini mtoto huyo ndiye atakayeleta amani katika ukoo husika kama kiongozi. Pia, huamini kuwa mtoto huyo amemaliza ugomvi kati ya mama wa mtoto na ukoo wa mume wake. Suala la mtoto wa kiume kuthaminiwa sana kuliko mtoto wa kike ni jambo linalojitokeza pia katika jamii nyingi za Kitanzania kama vile Wasukuma, Wakurya na Wamasai (Resani, 2012).

**e) Majina kutokana na Historia na Matukio mbalimbali**

Katika jamii ya Wabena kuna majina ambayo watoto hupewa kulingana na matukio yaliyotokea katika jamii yao kipindi fulani cha kihistoria; kwa mfano, matukio kama vile njaa, mvua, magonjwa, mafuriko na mengine kama hayo. Kwa mfano, *Mutonya* ni jina analopewa mtoto wa kiume ambaye amezaliwa wakati wa mvua. Hivyo kutokana na umuhimu wa mvua jamii ya Wabena iliweka kumbukumbu katika familia au jamii kwa kutoa jina hili kwa mtoto ambaye amezaliwa wakati wa tukio hilo. Pia, kwa watoto wa

kike waliozaliwa wakati wa mvua hupewa jina la *Mtonya*. Jina jingine kulingana na matukio ya kihistoria ni *Madzengo*. Jina hili hupewa mtoto hasa wa kiume aliyezaliwa wakati wa kukata miti ya kujengea nyumba hasa zile za miti. Miti hii hukatwa na wanaume mara nyingi ambapo wanawake hushirikishwa kusomba. Hivyo majina kama haya yana athari kubwa katika jamii hii kwani yanatunza kumbukumbu ya kihistoria ya utunzaji wa matukio.

Jina jingine ni *Nzalapamoto* ambalo maana yake ni njaa. Katika jamii ya Wabena jina hili hupewa watoto waliozaliwa wakati wa njaa, yaani kipindi ambacho watu hawana chakula cha kutosha. Kwa mfano, mwaka 1962 njaa ilitokea kwa sababu ya kuvamiwa na nzige ambao waliharibu mazao na kusababisha njaa. Hivyo jina hili linatunza historia ya jamii husika. Pia kuna jina *Dzosamagulu* ambalo humaanisha njaa iliyochosha miguu kutembea. Historia ya Wabena inaonyesha kuwa tukio la njaa lililotokea mwaka 1860 lilidhoofisha miguu ya watu kiasi cha kuwafanya washindwe kutembea umbali mrefu kutafuta chakula. Hivyo, majina haya walipewa watoto waliozaliwa katika misafara hiyo ya kutafuta chakula. Aidha, jina jingine la kihistoria lililotokana na tukio la njaa lililosababishwa na nzige walioharibu mimea ni *Makombele*. Jina hili humaanisha mtu mharibifu katika jamii. Hivyo katika jamii ya Wabena bado hukumbuka tukio hili na kuwapa majina watoto waliozaliwa kipindi hiki, na watu hawa ukubwani huwa wenye tabia ya uharibifu wa vitu jambo linaloonyesha kuwa majina yao yanawaakisi wakirejelea wadudu waliosababisha njaa kwa kuharibu chakula.

Majina mengine kulingana na tukio ni yale anayopewa mtu katika shughuli za kilimo cha ushirika. Katika jamii ya Wabena mwenye shamba huandaa pombe na huwaalika watu wengine waende kulima pamoja na kunywa pombe hiyo. Miongoni mwa majina yanayoibuka katika shughuli kama hizi ni kama vile *Ngufupamugovwe* na *Nguvuhudasi*. *Ngufupamugovwe* ni jina la kiume lenye kumaanisha bidii katika kazi ya kilimo cha ushirika na mtu anayekuwa wa kwanza kumaliza tuta. Hivyo kutokana na shughuli hizi jamii ya Wabena ilikuwa na desturi za kutoa mabinti zao kwa mume ambaye ataonyesha bidii katika kazi, yaani mwanamke hukaa mwishoni mwa shamba na atakayetangulia kumaliza ndiye atakayemwoa binti huyo. Katika jamii ya Wabena jina hili huwafanya wanajamii kuwa na bidii na kujituma katika kazi na kuleta maendeleo ya kilimo.

**f) Majina ya Watoto Waliozaliwa na Mama Aliyedhaniwa Hatazaa**

Katika jamii ya Wabena watu ambao hudhaniwa kuwa ni tasa kwa kuchelewa kuzaa huweza kudharauliwa, kunyanyaswa, kuchekwa na pengine kutengwa kabisa na jamii. Wanawake kama hawa inapotokea kuwa wamepata watoto, majina ya watoto hao huweza kuitwa: *Adziwikhe*, *Luhigilo*, *Luponelo* au *Abulumilwe.* Majina haya huonyesha bezo kwa wale wote waliomtukana na hata kumtenga mwanamke fulani kwa kuwa hazai. *Adziwikhe* humaanisha kuwa (Mungu) amenikumbuka, ameniondolea mkosi au aibu. *Abulumilwe* humaanisha (Mungu) ameniosha, na amenisafisha mikosi. *Luponelo* ni jina ambalo humaanisha kuwa miungu imemkumbuka mama huyu baada ya kukaa muda

mrefu bila kupata mtoto (amepona). *Luhigilo* humaanisha kuwa hukumu imeshaondolewa, kesi imemalizika au imefutwa, mhusika amesafishwa na kuondolewa mkosi. Jina hili hupewa mtoto wa kiume aliyezaliwa na mama aliyedhaniwa kuwa ni tasa na hawezi kuzaa. Jina hili humaanisha pia kwamba kile kitendo cha kutengwa na jamii kimekwisha kwa kuwa mtoto amezaliwa na amemaliza kabisa tatizo la mwanamke kutengwa na jamii yake kwani jamii bado ingali inaamini mwanamke ndiye tasa tu ila si mwanamume.

Kuhusiana na tatizo la uzazi kwa mwanamke pia jina *Shawodzidze* linatokana na muktadha huu. Jina hili humaanisha kuoza, kuharibika kisha kukauka. Katika jamii ya Wabena jina hili hupewa mtoto aliyezaliwa na mama ambaye alitumia dawa za asili ili kubeba mimba. Katika jamii ya Wabena mwanamke akiolewa hutegemea kuwa atapata mimba mapema na inapotokea anachelewa huweza kutumia dawa za asili (mitishamba) ili kuozesha/kutibu ugonjwa ambao pengine upo tumboni ili aweze kupata mimba. Hivyo, mama huyo akifuata masharti ya kutumia dawa hiyo na ikamsaidia akapata mimba na akaweza kumzaa mtoto basi huyo hupewa jina la *Shawodzidze*. Jina hili hutunza kumbukumbu ya kuwa mama wa mtoto katika familia fulani alikumbwa na tatizo la kutokupata mimba kwa hali ya kawaida.

**g) Majina kwa Watoto Waliozaliwa Ugenini**

Katika jamii ya Wabena kuna majina ambayo watoto hupewa ikiwa wazazi wao wamewazaa wakiwa maeneo ya ugenini. Wazazi hao wanaweza kuwa ugenini kutokana na sababu mbalimbali kama vile njaa, biashara, ajira, shughuli za kidini, na vita. Sababu hizi huweza kuzifanya familia zao zikaendelea kuzaa na kuongezeka wakiwa katika nchi au maeneo ya ugenini (yaani mbali na maeneo yao ya asili). Katika mazingira kama hayo watoto wanaozaliwa ugenini huweza kupewa majina kama vile *Tulimwikhala*, *Twidewulye*, *Tulatang'ana* na *Lughendo/Maghendo*.

*Tulimwikhala* ni jina ambalo humaanisha kuwa porini, yaani nje ya eneo la asili ya mhusika. Hali kama hii hutunza kumbukumbu ya kuwa kuna wakati familia hiyo ilikuwa ugenini. *Twidewulye* ni jina ambalo lina maana kuwa tumejisahau, tumetulia na kuridhika kuishi ugenini. Jina hili linaonyesha jinsi familia hiyo ilivyokuwa ugenini hata ikajisahau kumrudisha mama mjamzito nyumbani kwao ili akajifungue. Katika taratibu za Wabena kipindi mama akiwa mjamzito na muda unakaribia kujifungua na yupo ugenini anatakiwa kurudi nyumbani ili aweze kujifungulia huko. Hivyo basi mama huyo akikaa ugenini mpaka akajifungua huko basi wanafamilia huwabeza wazazi wa mtoto na humpa mtoto jina la *Twidewulye*. Lengo la kumpatia mtoto jina hilo ni kutunza kumbukumbu ya kuwa alizaliwa ugenini nje na nyumbani kwao. Pia, ni onyo kwa famila za Wabena kupotelea ugenini, ni kama kuwaamsha na kuwakumbusha kurudi nyumbani.

Jina jingine ni *Tulatang'ana* ambalo hupewa mtoto aliyezaliwa ugenini, likimaanisha kuwa kuna ndugu ambao hawapo katika eneo ambalo mtoto huyo amezaliwa lakini huamini kuwa ipo siku atarudi na kukutana nao. Jina hili hutunza kumbukumbu ya kuwa familia husika ilikuwa nje na mazingira yake ya asili. *Lugendo/Magendo* pia ni jina katika jamii ya Wabena ambalo humaanisha kusafiri na kutembea umbali mrefu. Jina hili hutolewa kwa lengo la kutunza kumbukumbu kuwa mtoto husika alizaliwa kipindi wazazi wake wapo safarini.

**h) Majina kutokana na Matatizo na Vifo katika Familia**

Utafiti huu umebaini kuwa katika jamii ya Wabena kumekuwa na utaratibu wa kupeana majina kwa kuangalia nyakati na matukio yake. Mtoto aliyezaliwa wakati wa matatizo fulani katika ukoo au familia husika huweza kupewa jina linalosadifu tatizo hilo. Watoto wanaozaliwa katika kipindi cha matatizo hupewa majina kama vile *Lupumukho*, *Twilolela*, *Lumbwene* na *Lukulaso*. *Lupumukho* ni jina ambalo hupewa mtoto likiwa na maana ya mateso. Jina hili huonyesha jinsi mtoto husika alivyozaliwa kwa mateso. Kwa mfano inaweza kutokea kuwa mama aliugua kwa muda mrefu wakati wa ujauzito au kulitokea vita wakati mama huyo akiwa mjamzito. Lengo la kutoa jina hilo ni kuweka kumbukumbu katika familia kuhusiana na matatizo hayo. *Twilolela* ni jina lenye maana kuwa tutaona. Mtoto hupewa jina hili endapo amezaliwa katika hali fulani ambayo si ya kawaida. Kwa hali ya kawaida, watoto huzaliwa kwa kutanguliza kichwa lakini huwa inatokea mtoto mwingine huzaliwa akiwa ametanguliza miguu. *Lumbwene* ni jina wanalopewa watoto katika jamii ya Wabena likiwa na maana kuwa yamenikuta. Watoto hupewa jina kama hili ikitokea kuwa jamii iko katika matatizo fulani kwa mfano pengine baba aliumwa sana kabla mtoto hajazaliwa au mama wa mtoto alipasuliwa wakati wa kujifungua, basi mtoto huyo hupewa jina la *Lumbwene*. Lengo ni kutunza kumbukumbu kuwa familia ilikuwa na matatizo fulani wakati wa kuzaliwa kwa mtoto husika.

Katika jamii ya Wabena kuna majina ambayo hupewa watoto waliozaliwa wakati familia imekumbwa na tatizo la mtoto kufariki wakati wa kuzaliwa. Hivyo mtoto anayefuata hupewa jina fulani kama ishara ya utakaso kwa wale watakaozaliwa baadaye. Wazazi hutoa majina hayo ili kuondokana na laana au bahati mbaya ya vifo kuikumba familia au ukoo wao. Majina ambayo watoto hawa hupewa ni kama vile *Tuliwonda*, *Tulipamwinga* na *Tulilumwi* (yana maana kisawe yaani tuko pamoja). Majina haya kwa ujumla humaanisha kuwa hakuna atakayekwepa kifo, hata sisi tutapitia kifo. Hivyo majina haya hupewa watoto kama liwazo na faraja katika jamii kuwa wasijisikie wapweke. Lengo jingine la kuwapatia majina hayo ni kutunza kumbukumbu za kifamilia na pia kuomba mizimu tatizo hilo lisitokee kwa kizazi kijacho.

Jina jingine katika kundi hili ni *Tuladzifikha* lenye maana kuwa tutafika. Jina hili hupewa mtoto aliyezaliwa katika familia yenye matatizo kama ya kifo ambayo yaliikumba familia yake. Wabena huamini kuwa watu waliokufa hutangulia mbinguni

kuandaa makao ya milele hivyo wengine wanaofuata baadaye hukuta kumeandaliwa. Jamii hii huamini kuwa kizazi kitakachofuata kiondokane na tatizo hilo na watoto wanaozaliwa wabakie kuwa hai. Jina jingine ni *Anyamadze* ambalo humaanisha kuliwaza, kunyamazisha na kutoa suluhisho. Katika jamii hii hutoa jina hili ili kumnyamazisha mtu anayelia au kusononeka baada ya kukumbwa na tatizo fulani katika maisha yake kama vile kifo au ajali. Mtoto anayepewa jina hili huwa kitambulisho kuwa familia fulani ilikuwa na matatizo lakini kwa sasa yamekwisha. Aidha, *Dzing'ula* ni jina lenye maana ya kunungu'nika. Katika jamii ya Wabena mtoto anayezaliwa wakati familia ina migogoro, yaani kati ya baba na mama wakishindwa kuelewana anapewa jina hilo ili kutunza kumbukumbu kuwa familia yao ilikuwa na matatizo katika kipindi fulani. Athari ya jina hilo katika jamii ya Wabena ni kwamba mtu anaweza kufa kutokana na manung'uniko na pengine kusababisha mikosi kwa wengine. Hivyo wazee wa Kibena hukaa na kutatua matatizo kama haya ili kuondoa mikosi ambayo inaweza kukumba familia itakayofuata kwa kufanya matambiko ya kimila.

**i) Majina kwa Watoto Waliozaliwa Pekee**

Katika utafiti huu imebainika kuwa katika jamii ya Wabena kuna majina ambayo huweza kupewa watoto ambao wamezaliwa peke yao bila kuwa na ndugu yeyote wa kuzaliwa naye yaani dada, kaka, wala mdogo wake. Majina haya hutolewa ukubwani baada ya wazazi kukata tamaa kuwa hatazaliwa mtoto mwingine baada yake. Jina hili la pili la ukubwani mara nyingi hujulikana kwa watu wa ukoo wa mhusika. Baadhi ya majina haya ni kama vile *Alimwene* au *Aliyuyo* ni miongoni mwa majina yanayomaanisha kuwa yupo peke yake. Pia, *Mugayalukolo* ni jina jingine lenye maana sawa na hiyo (hana ndugu wa kuzaliwa naye). Kwa kawaida majina haya (*Alimwene*, *Aliyuyo* na *Mugayalukolo*) hutolewa na wazazi wa mtoto aliyezaliwa baada ya wao kukata tamaa kutokana na sababu mbalimbali za uzazi kugoma.

**j) Majina Kutokana na Sifa ya Mzazi**

Katika jamii ya Wabena, kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika, kuna majina ambayo watu hupewa kulingana na sifa za wazazi wao. Mathalani, jina *Mpingwa* ambalo humaanisha mtu ambaye hana shida ya chakula, fedha za matumizi na mwenye tabia ya kutoa misaada kwa wenye shida. Jina hili hupewa watoto wa kiume tu ambao wamezaliwa katika familia tajiri na ambao katika jamii yao ikitokea kuna tatizo hujitolea kwa misaada kuwasaidia wengine. Jina hili linatukumbusha kwamba ikitokea mtoto huyo akapata tatizo basi asaidiwe na mtu yeyote kwa kuwa wazazi wake waliwasaidia pia watu wengine wakati wa shida. Pia, majina ya *Lunodzo* na *Amodzidze* yana maana hiyo hiyo; ni visawe vya jina hilo.

Aidha, *Fyungupamoto* ni jina lenye maana ya mtu mwongo. Jina hili hupewa mtu ambaye huwa na maneno mengi ya uongo na ya kugombanisha watu katika jamii. Hivyo katika familia kama mama wa mtoto huyo alikuwa na jina hilo basi mtoto wake wa kwanza au atakayefuata anaweza kupewa jina hilo. Athari ya kurithisha majina haya ni

kwamba huendeleza imani ya tabia mbaya katika jamii maana watu huamini kwa maneno. Na kutokana na utafiti huu, watoto wengi hukataa majina haya ukubwani mara baada ya kujitambua na kujua maana ya majina yake.

**k) Majina yatokanayo na Dini ya Kikristo**

Baada ya ujio wa wageni hasa Wajerumani waliokuja kutawala kati ya 1900-1914, Wabena wengi waliingia na kuathiriwa na utamaduni wa kigeni, ikiwemo dini ya Kikristo. Hivyo, kwa sehemu kubwa Wabena waliacha kuwapa watoto wao majina ya asili na kuwapa majina ya kigeni. Majina mengi yakawa ni ya kumsifu, kumtukuza, na kumfurahisha Mungu ambayo yanapatikana katika Biblia takatifu. Kwa mfano, katika lugha ya Kibena jina *Alatusunguhiye* huashiria huruma ya Mungu. Jina hili lina maana kuwa ni kwa huruma ya Mungu pekee ndipo jambo fulani huweza kufanyika na kufanikiwa. Aidha, *Lusungu* maana yake ni huruma. Watoto wengi katika jamii ya Wakristo hupewa majina haya wakiwa na lengo kubwa la kuitambulisha jamii juu ya huruma na neema za Mungu na kuweza kuwavuta wanajamii wengi kufuata neno la Mungu na kuishi maisha ya kumtegemea Mungu. Majina mengine ni kama vile *Twilumba* lenye maana ya tunakushuru Mungu kwa matendo yako makuu. *Alumbwage* lenye maana ashukuriwe Mungu, *Tulahkela* lenye maana tutafurahi kwa pamoja nawe Mungu, *Alanyamanza* lenye maana ataninyamazisha katika kilio changu, na *Anzimilye* lenye maana ya amenisimamia katika mambo yangu.

**l) Majina ya Kurithi**

Jamii ya Wabena pamoja na kwamba iliingiliwa na dini za kigeni (Ukiristo na Uislamu) na kuweza kuiga au kubadili utamaduni, lakini bado wanauenzi utamaduni wao kwa kurithishana majina kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Jamii nyingi za Kiafrika, kama asemavyo Hountondji (1977), zinasisitiza uviringo katika maisha yao. Hountondji anaeleza kuwa Waafrika huamini kifo ni pumziko la muda lakini baadaye binadamu hufufuka kupitia uzao wa watoto katika jamii yake, nao wanapopewa jina la marehemu inakuwa ni kama marehemu kafufuka na kuanza maisha upya. Wabena nao wana uviringo katika kupeana majina na kulingana na falsafa hii ya Kiafrika ya uviringo, huamini majina ya mababu hurithishwa kwa watoto ili kuwafanya mababu waendelee kuwapo. Utafiti huu umebaini kuwapo kwa sababu mbalimbali za kuwapo kwa urithi wa majina, sababu hizo ni Mosi, familia hutoa jina na kumpatia mtoto baada ya kutambua mchango wa aliyerithiwa jina hilo. Pili, kumfanya mwanafamilia aliyerithiwa jina aendelee kuwapo japo amekufa. Jamii ya Wabena huamini kuwa kwa kumrithisha mtoto jina la ndugu aliyefariki ataendelea kuishi ndani ya yule mtoto aliyerithi jina. Tatu, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu kuhusu kizazi kilichotangulia. Mtoto huweza kupewa jina la babu, bibi, mjomba, kaka, shangazi na ndugu wowote katika ukoo au familia. Pia, wazazi huchagua tabia zinazoendana baina ya mtoto na anayerithiwa jina hilo na hii huenda ndiyo sababu ya baadhi ya majina hayabadiliki kama majina ya ukoo.

**m) Majina kwa Wanajamii wenye Imani za Kishirikina au Kichawi**

Wabena, huamini kuwa katika jamii yao upo ushirikina na uchawi. Mara nyingi katika jamii ya Wabena watu wenye tabia ya uchawi hupewa majina mbalimbali yenye kuwatambulisha kuwa siyo watu wazuri katika jamii, na mara nyingi hupewa majina haya ukubwani. Majina haya huanza kisiri siri ndani ya jamii lakini baadaye huachwa yajulikane kama ishara ya kumwambia mwenye jina kuwa jamii inamfahamu na tabia zake. Majina ambayo watu wenye tabia hiyo hupewa ni kama vile *Pongolivakha* ambalo humaanisha mbuzi mkubwa dume; yaani *Pongo* ni mbuzi dume na *Livakha* ni kubwa na iliyokula chumvi nyingi. Kwa kawaida, mbuzi dume ana uwezo mkubwa wa kupambana na huogopwa na mbuzi wengine wadogo. Hivyo, katika jamii ya Wabena mtu anayesemekana kuwa na imani za kishirikina hufananishwa na mbuzi mkubwa au beberu ambaye huogopwa na watu wengine katika jamii. Lengo la kutoa jina kama hili kwa mtu mwenye tabia ya ushirikina ni kutaka kumkejeli kwa tabia zake alizonazo. Watu wanaopewa majina haya huweza kutengwa na jamii kwa sababu wanaaminika kuwa ni wauaji. Pia, majina kama haya huwa ni kumbukumbu katika familia au jamii kwa vizazi vijavyo viweze kufahamu na pia kuepukana na tabia kama hizo na fedheha ya kupewa jina chafu ukubwani**.**

Aidha, kuna majina ya utani kuhusiana na mtu anayehisiwa kuwa ni mchawi, majina hayo ni pamoja na *Ngongomi* na *Madonga*. Mathalani, jina *Ngongomi* hupewa mtu anayedhaniwa kuwa na tabia ya ushirikina au uchawi. *Ngongomi* maana yake ni jogoo mzee anayeogopwa na jogoo wengine ndani na nje ya mtaa wake. Jamii ya Wabena hutoa majina haya kwa lengo ka kutambulisha tabia ya mtu fulani kwa jamii ili iweze kujihadhari naye. Jina hili huweza kumfanya mtu aliyepewa kutengwa na kuogopwa na wale wasio wachawi kwani huchukuliwa kuwa ni kweli. Lakini wakati mwingine haya ni majina ya ukubwani wapewayo watu baada ya jamii kuona mienendo na mielekeo yao ya maisha.

*Madonga* ni jina jingine la utani ambalo hupewa mtu anayeonekana kuwa na tabia hii ya ushirikina/uchawi. *Madonga* lina maana ya rungu kubwa ambalo hutumika kuwindia wanyama na kuchungia mifugo mbalimbali kama ng’ombe, mbuzi na kadhalika. Jina hili hulinganishwa na mtu mwenye tabia ya ushirikina kwa kuwa akikufanyia uchawi wake maumivu ni sawa na kupigwa na rungu kubwa ambalo mwindaji hutumia kuulia wanyama na adui mawindoni. Kwa kutumia jina hili jamii husisitizwa kujitenga na wenye tabia hii na vizazi vijavyo visiweze kuiga au kupewa majina kama hayo kwani hayapendwi katika jamii na siyo mazuri kwa urithi wa vizazi vijavyo. Hivyo, jamii ya Wabena hutoa majina haya ili kuepusha urithi mbaya kwa vizazi vijavyo na kumkejeli mhusika mwenye tabia hii kwani pindi anapogundua kuwa watu wanajua yeye ni mchawi anaweza kupunguza ama kuacha kabisa.

## 3.0 Hitimisho

Kwa jumla tunaweza kusema kuwa lugha, kama chombo cha kuwezesha mawasiliano katika jamii ya watu wenye utamaduni mmoja, huweza kutumika katika kupeana majina kwa ujumla wake. Kila jina la wanajamii huwa na maana fulani. Maana hii ndiyo inayotufanya tumfahamu mhusika kwa kina. Pia, tunatoa wito kwa wanazuoni kuendelea kutafiti na kukuza lugha zetu za asili kwani tusipohifadhi lugha zetu hasa katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia basi kuna hatari ya kuzipoteza lugha zetu za asili kwa kuwa hazitakuwa na watumiaji. Pia Kiswahili kinakuwa kwa kasi na kinatishia lugha zetu za Kibantu kwa hiyo kuziandika inapaswa kuwa ni wajibu wetu sisi wasomi.

## Marejeleo

Besha, R. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Buberwa, A (2010). Upekee wa Nomino Mahususi: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Mahali ya Kihaya, *Kioo cha Lugha* Juz. 8: 9-15.

Enhret, E. (1958). *Language and Culture*. New York: Ohio University.

Habwe, J. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hountondji, P. (1977). Sur la philosophie africaine. Paris: Maspero *(African Philosophy: Myth and Reality*. Bloomington: Indiana University Press, 1983).

Guthrie, M. (1948). *The classification of Bantu Language*. London: Oxford University Press.

Kihore, Y. M na wenzake. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Kibiki, A.S. (2013). Dhima ya Lakabu katika Kupeana Majina katika Jamii ya Wabena. Tasnifu ya Digrii ya Uzamivu katika Fasihi. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kilimile, M. (2009). Hadithi na Masimulizi ya Wabena. Phoenix Publishers.

Kipacha, A. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu.* Dar es Salaam: Open Univesity of Tanzania.

Massamba na wenzake. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu. Sekondari na vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mphande, L. (2006). *Naming and Linguistic Africanism in Africa-American Culture*. New York: Ohio University.

Msanjila, A. (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Muzale, H.R.T. (1998). Linguistic and Social Cultural Aspects of Interlacustrine Bantu Names, *Kiswahili*, Vol. 61:28-52

Nuso na Mgaya (tarehe 12/3/2015) Masimulizi ya Mdomo, Njombe Mjini.

Nyagava, I. (1988). The History of the Bena up to 1908, Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nyagava, I. (1994). *The Historyof the Bena*. University Committee for Development Reaserch. London.

Resani, M. (2012). Sociolinguistic and Semantic Analysis of Kurya Personal Names, Tasnifu ya Umahiri ( haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dodoma.